**MASOMO YA BIBLIA YA KIKRISTADELFIA KWA NJIA YA POSTA**

# NAMNA YA KUITUMIA KOZI HII YA BIBLIA

**SOMO:** Zaburi 19

Kozi hii imeandaliwa ili kukusaidia uweze kuielewa Biblia, ambayo ni Neno la Mungu. Biblia, ambayo pia huitwa “Maandiko”, ndio kitabu pekee kinachoweza kuaminika, kutuambia juu ya Mungu na mpango wake kwa dunia, na kwa watu wanaoishi juu yake. Inatoa ahadi ya mbaraka kwa kila mtu anayeisoma, akiwa na nia ya dhati ya kuielewa.

**Utahitaji kuwa na Biblia yako mwenyewe**
Ni fursa ya bahati kuwa na nakala ya Neno la Mungu. Ili kuifuatilia vizuri kozi hii, utahitaji kuwa na nakala yako mwenyewe ya Biblia yote (na sio Agano Jipya tu). Kama bado hujawa nayo, unaweza kupata moja kwa bei ambayo sio kubwa, kutoka kwenye tawi la karibu la Chama cha Biblia, au katika maduka ya vitabu. Karibu kila nchi ina tawi la Chama hicho. Lakini, kama hili haliko chini ya uwezo wako, tafadhali mwambie mkufunzi wako haraka; anaweza kukusaidia pengine kupata hata iliyotumika.

Masomo haya kwa njia ya Posta yana mada 60, moja kwa kila juma. Kama mkufunzi wako (mtu anayekutumia masomo haya) anaishi mbali na wewe, inawezekana kuwa utapata masomo kadhaa pamoja, pamoja na karatasi za maswali, pengine mara moja kwa mwezi. Mkufunzi wako ni:

________________________________________________
________________________________________________
________________________________________________
________________________________________________
________________________________________________
________________________________________________

**Kumbukumbu yako itakuwa namba: _______________**
Tafadhali utumie namba yako hii kwa mawasiliano yote, kwenye karatasi za majibu, n.k.

Tunakuomba utume majibu yako yote (na maswali uliyonayo) kwa mkufunzi wako. Ingekuwa vizuri zaidi umwandikie mkufunzi wako tu, hata kama unaona kuna anwani zingine kwenye machapisho yetu.

Kama utapenda pia kutumia Biblia ya Kiingereza, nukulu zilizowekwa zipo katika Biblia ya Kiingereza ya ‘Authorized Version’. Yapo machapisho mengine ya kisasa zaidi, kama ‘Revised Standard Version’ na ‘New International Version’, lakini yanaweza yasiwepo katika baadhi

ya nchi. Hata hivyo yoyote ile utakayoitumia, utaona haitabadilisha maana au kuathiri kujifunza kwako Biblia.

Mafundisho haya tunayatoa bure. Gharama pekee utakayoingia ni kulipia gharama ya kutuma barua yako kwa mkufunzi wako, mara moja kwa mwezi. Lengo letu ni kukusaidia wewe kufurahia kuyasoma Maandiko, na tunatamani uweze kuugundua ujumbe wa maana sana na wokovu ulioko ndani yake, kupitia kwa Yesu Kristo. Hatutoi vyeti au hati yoyote kwa kuichukua kozi hii, ila mwishoni mwa masomo haya 60 tungependa bado tuendelee kukusaidia kuendelea kujifunza Biblia yako.

**Rejea za Biblia**

'Rejea' kutoka kwenye Biblia itakapokuwa imetolewa, itakuwa imeandikwa ifuatavyo:

> Mwanzo 1 – hii ina maana ya Kitabu cha Mwanzo, Sura ya 1.
> Mwanzo 1:1-7 ina maana ya Kitabu cha Mwanzo, Sura ya 1,
> mstari wa 1 mpaka wa 7 (mstari wa 7 unahusika).

**Namna ya kujifunza masomo haya**

Jizoeze kufanya mada moja kila juma. Tungeonelea uhakikishe unaielewa kila mada, kabla hujaendelea na nyingine inayofuata. Unaweza ukaona ni kitu cha manufaa kupitia kila mada **mara tatu**. Mara ya kwanza kwa kutaka kupata wazo la jumla la kile kinachosemwa, mara ya pili kwa kuifungua Biblia yako kwenye rejea zilizotolewa, na kuandika kwa kifupi kwenye kipande cha karatasi tatizo unaloliona au swali, na mara ya tatu kuisoma tena mada yote. Ni vizuri katika hatua hii kulisoma SOMO la Biblia lilitolewa mwanzoni mwa mada hiyo.

Mwishoni mwa kila mada utaona mistari ya manufaa ya kutazama kwenye Biblia yako, na Andiko moja tunalokutaka hasa kuliweka moyoni. Utaona kuwa, mistari hii itabakia kwenye kumbukumbu yako na itakusaidia katika maisha yako yote.

Pamoja na karatasi zako za mada za kwanza utakazopewa, utapewa pia na 'Mpango wa Kujisomea Biblia wa Kila Siku', tunaouita BIBLE READING PLANNER (kwa Kingereza). Kijitabu hiki kitakupa mfumo wa namna ya kusoma Biblia, kwa kusoma kifungu kimoja **kila siku**. Kama utakuwa na utayari wa kufanya hivyo, utapata ufahamu mzuri wa sehemu zote za Biblia baada ya muda.

Unaweza kupenda kuweka Mpango wako huo ndani ya Biblia yako, kwa ajili ya kuutumia wakati wa kusoma kila siku. Hili ni jambo jema. Kijitabu hiki kina maoni kinayokupa juu ya vifungu hivyo unavyosoma kila siku; na hasa ni muhtasari wa kile ulichosoma. Kina rejea za mistari mingine ya kwenye Maandiko, na ramani ndogo ndogo na michoro, inayoweza kukusaidia katika kujifunza kwako.

**Kujibu maswali**

Tunakutaka utume majibu yako kwa mkufunzi wako kila mwezi. Unatakiwa ujibu kwa kutumia maneno yako, usinakili tu kile masomo yalichosema. Jaribu kusema kile unachoamini mwenyewe kuwa kweli. Kama hukubaliani na chochote unachosoma, au una maswali yoyote, tafadhali sema hivyo; hili ni jambo la muhimu sana. Kumbuka, tunaweza kukusaidia zaidi kama tukiwa tunajua unachofikiri. Kama kwa sababu yoyote huwezi kutuma majibu yako, basi mwandikie tu mkufunzi wako kumwambia unapenda kuendelea na masomo.

**Matumizi ya muda**
Kwa vyovyote, kujifunza huku kutakuchukulia sehemu ya muda wako, pengine dakika 15 au 20 kila siku kwa kusoma somo lako la Biblia, na kama nusu saa kwa kujifunza mada uliyopewa. Utahitaji pia muda wa kujibu karatasi za maswali. Hata hivyo utagundua kuwa, Maandiko yanavutia kiasi kwamba utahitaji kutumia muda wa zaidi na zaidi kuyapitia.

Soma Biblia yako kwa kuomba. Anza kipindi cha kusoma Biblia au kujifunza kwa kumwomba Mungu, ukiomba msaada wake uweze kuelewa. Hapa kuna ombi fupi kutoka katika Kitabu cha Zaburi:

> “Uyafumbue macho yangu niyatazame maajabu yatokayo katika sheria yako” (Zaburi 119:18).

Kama tukimwomba Mungu kwa dhati, atayafungua macho yetu na kutusaidia kukielewa kitabu chake hiki cha muhimu sana kwetu.

**Kama hatutasikia kutoka kwako**
Tuna hakika utakuwa unaelewa kuwa, kuna watu wengi duniani humu wanaotamani kuipata kozi hii ya Biblia. Kama hatupati mwitikio wowote kutoka kwako, kwa wewe kututumia majibu ya karatasi za maswali ulizopata, tutachukulia kuwa huhitaji tena kuendelea kupata masomo haya na tutaacha kuendelea kuyatuma kwako.

Kama una matatizo yoyote katika kujibu, au katika kutuma karatasi zilizojibiwa, tafadhali wasiliana na mkufunzi wako umweleze. Itakuwa ni furaha kwetu kuendelea kukutumia masomo. Tunachohitaji tu ni kujua kama yanakufikia, na umekuwa ukiyatumia kukusaidia katika kujifunza kwako Neno la Mungu.

**Kozi kamili ya Biblia:**
Ifuatayo ni orodha ya mada ya kila somo, katika kozi hii ya masomo 60

1. Namna ya Kuitumia Kozi Hii ya Biblia
2. Wakristadelfia ni Watu Gani?
3. Mwongozo Wetu Biblia

4. Injili

Karatasi ya Maswali Na. 1

5. Mungu na Uumbaji
6. Mungu Aliupenda Ulimwengu
7. Kurudi kwa Bwana Yesu Duniani
8. Ishara za Kurudi kwa Yesu

Karatasi ya Maswali Na. 2

9. ‘Ufalme Wako Uje’
10. Mungu anavyoiona Historia
11. Ufalme wa Mungu – Amani Duniani

Karatasi ya Maswali Na. 3

12. Ahadi za Mungu  kwa Ibrahimu
13. Wayahudi katika Historia (Sehemu ya 1)
14. Wayahudi katika Historia (Sehemu ya 2)
15. Ahadi za Mungu kwa Daudi

Karatasi ya Maswali Na. 4

16. Baba na Mwana
17. Maisha ya Yesu
18. Kifo cha Yesu
19. Ufufuo na Kupaa kwa Yesu Kristo

Karatasi ya Maswali Na. 5

20. Roho Mtakatifu wa Mungu
21. Karama za Roho Mtakatifu
22. Dhambi na Matokeo yake (Sehemu ya 1)
23. Dhambi  na Matokeo yake (sehemu ya 2)

Karatasi ya Maswali Na. 6

24. Kwa Neema Mmeokolewa
25. Ufufuo wa Wafu
26. Hukumu
27. Uzima wa Milele

Karatasi ya Maswali Na. 7

28. Malaika
29. Ibilisi, Mapepo, Shetani
30. Ibilisi na Dhambi
31. Ubatizo

Karatasi ya Maswali Na. 8

32. Ndoa ya Kikristo
33. Matatizo katika Ndoa
34. Wajibu Wetu kwa Taifa
35. Maombi
36. Kutembea Katika Njia ya Uzima

Karatasi ya Maswali Na. 9

37. Usomaji wa Biblia wa Kila Siku
38. Ushirika na Walio wa Imani moja
39. Uwezo wa Ulimi
40. Kumega Mkate

Karatasi ya Maswali Na. 10

41. Maisha ya Kifamilia katika Huduma ya Yesu
42. Tatizo la Dhambi
43. Neno la Mungu katika Maisha yetu ya Kila Siku
44. Kanisa la Mungu

Karatasi ya Maswali Na. 11

45. Tunavyowafikiria Wengine ni Muhimu kwa Mungu
46. Kumpenda Jirani Yako
47. Biblia Inavyosema Juu ya Mateso
48. Kuishi kwa Hofu

Karatasi ya Maswali Na. 12

49. Ni Sahihi Kupenda Makuu?
50. Uaminifu kwa Mungu na Mwanawe, Yesu Kristo
51. Matumizi na Udhibiti wa Hasira
52. Mfuasi na Nchi

Karatasi ya Maswali Na. 13

53. Kufanya Mapenzi: zawadi kutoka kwa Mungu
54. Kuchagua Mchumba
55. Vipengere kuhusu Hukumu na Ufalme wa Mungu
56. Zawadi ya Thamani Kubwa ya Tumaini katika Maisha yako

Karatasi ya Maswali Na. 14

57. Imani na Kuufanyia Kazi Ukristo
58. Neema ya Mungu
59. Muhtasari wa Mafundisho ya Biblia

60. Hatua Inayofuata

Karatasi ya Maswali ya Mwisho